

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI

15 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI – TAREHE 15 APRILI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**79. MHESHIMIWA VICENT PAUL MBOGO
(NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Nkasi Kusini lina Kata 11 na Kituo cha Afya kimoja pekee:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Vituo vya Afya hasa katika Tarafa ya Chala, Kate, Myula, Sintali na Ninde.

**80. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):

Je, ni lini Serikali itakamilisha ununuzi wa Vifaa Tiba ikiwemo vya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Mwabayanda Wilayani Maswa.

81. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sera ya Matibabu Bure kwa Wazee wenye umri kuanzia miaka 60 katika Halmashauri za Mkoa wa Mara inatekelezeka.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:



82. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Masisiwe, Nyanzwa, Irole na Ibumu ambazo zina shida kubwa ya mawasiliano.

WIZARA YA MAJI:

83. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Kijiografia Tanzania ipo kwenye Ukanda
wenye mvua za kutosha:-

Je, Serikali imejizatiti vipi kuhamasisha zoezi
la uvunaji maji ya mvua kwa matumizi ya
Wananchi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri
Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
15 April, 2021

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE